USAFIRI

# Wadau wataja mwendokasi waitakayo

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchi@mwananchi.co.tz



Abiria wakiwa katika foleni ya kupanda magari ya mwendokasi katika Kituo cha Kimara jijini Dar es Salaam jana. **Picha na Michael Matemanga**

**Dar es Salaam.** Siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuteua watendaji na bodi mpya za taasisi zinazosimamia na kuendesha mradi wa mabasi yaendayo haraka, wadau wanaeleza kazi iliyo mbele yao, huku wakitaka mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji, ili kufikia matarajio ya wananchi.

Aidha, mabasi yaliyoongezwa kwa muda kuanzia juzi katika njia ya Kivukoni-Mbezi, yametajwa kuleta ahueni kwa wasafiri waliokuwa wanakabiliwa na kero kubwa ya usafiri.

Mradi wa BRT ulianzishwa kwa lengo la kuondoa kero ya msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, tangu ulipoanza huduma katika awamu ya kwanza ya ujenzi (njia ya Mbezi – Kivukoni), haukuwa na ufanisi wala kufikia malengo yaliyotarajiwa.

Watendaji wa taasisi zinazosimamia mradi huo, wamebadilishwa mara kadhaa na juzi, Rais Samia alitengua uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), Athumani Kihamia na yule wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (Udart), Waziri Kindamba.

Badala yao, aliwateua Said Tunda kuchukua nafasi ya Kihamia na Pius Ng'ingo kwa nafasi ya Kindamba. Vilevile, ameteua wenyeviti wa bodi; David Kafulila (Dart) na Ramadhan Dau (Udart).

Kwa mujibu wa wadau waliozungumza na *Mwananchi* jana, walisema kuna haja ya kurejea kwenye malengo ya kuanzishwa kwa mradi huo na kutengeneza muundo utakaotoa matokeo yanayotarajiwa.

Profesa Abel Kinyondo, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema mabadiliko yaliyofanyika ni uamuzi wenye mrengo chanya kwa sababu ni hatua ya mwanzo ya kufanyia kazi matatizo yaliyopo kwenye mradi huo.

> **"Ifike mahala, mtu anapoteuliwa awe anawajibika... kwa nini wasiweke ushindani, kwamba nafasi hii ya mkurugenzi itangazwe, watu waje na uzoefu wao na akikabidhiwa pale, apewe target (malengo), akiweza apewe bonasi, asipoweza anafutwa kazi mara moja."**
>
> Dk Onesmo Kyauke

Hata hivyo, alisema si mara ya kwanza mabadiliko kama hayo yanafanyika, akieleza kikubwa ni kwa namna gani mabadiliko hayo yataleta maendeleo endelevu.

Alisema watendaji wapya ni kama wanakwenda kuanza upya kwa kuangalia malengo ya kuanzisha Udart na Dart. "Lengo la kwanza lilikuwa 'tukianzisha Dart, tutatoa huduma ya usafiri ambayo ni ngazi ya juu kiasi kwamba si tu watu watawahi kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini hata mwenye gari binafsi atapaki gari lake kwa sababu anaona akilitumia, gharama ni kubwa," amesema.

Mbali na hilo, mtaalamu wa uchumi, Oscar Mkude, alisema tatizo kubwa ni muundo wa mradi kwani ulipoanzishwa ulitakiwa upate mwendeshaji mwenye uwezo wa kifedha na uzoefu wa kuuendesha katika mfumo wa ubia kati ya sekta binafsi na Serikali (PPP).

"Sasa, huyo mwendeshaji hakupatikana, badala yake Udart wakajiweka kama waendeshaji. Hapo siasa zikaanza kuchezwa, Udart wakapewa kuwa waendeshaji wa mpito wakati mazingira ya kupata mtaalamu yanaendelea, hapo ndipo mambo yakaanza kubadilika," alisema.

Mkude alipendekeza watendaji wapya wapewe kipimo cha utendaji wao (KPI) ndani ya muda fulani ili kuleta matokeo. Pia, muundo wa uendeshaji wa mradi ubadilishwe ili kuleta tija.

Kwa upande wake, Dk Onesmo Kyauke, yeye alisema mradi wa BRT ulianza vizuri na sasa magari mengi yamekufa kutokana na usimamizi mbovu, hivyo amependekeza mabadiliko katika mifumo ya udhibiti.

Alisema uongozi mpya una kazi ya kuhakikisha magari mapya ya kutosha yanapatikana kwenye mradi huo na kuhakikisha mifumo ya kidijitali inatumika hasa kwenye ukataji wa tiketi kwa abiria.

"Ifike mahala, mtu anapoteuliwa awe anawajibika... kwa nini wasiweke ushindani, kwamba nafasi hii ya mkurugenzi itangazwe, watu waje na uzoefu wao na akikabidhiwa pale, apewe target (malengo), akiweza apewe bonasi, asipoweza anafutwa kazi mara moja," alisema.

Wakati wachumi wakipendekeza hayo, baadhi ya wananchi wamepongeza uamuzi wa Serikali na Kampuni ya Mofat Limited kuanza kutoa huduma katika Barabara ya Morogoro.

Juzi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema mabasi mapya 60 yanayopaswa kutumika katika mradi wa Mbagala yameongezwa ili kutatua changamoto iliyokuwapo barabara ya Morogoro iliyokuwa imesalia na mabasi 30 pekee.

Mwananchi ilishuhudia abiria wachache vituoni wanaosubiri mabasi, tofauti na ilivyokuwa awali waliposubiri kwa zaidi ya saa moja.

Mfanyabiashara wa samaki, mkazi wa Kimara, Tatu Rajab alisema: "Nilikuwa nikija kuchukua samaki nakaa muda mrefu kituoni, kwa sasa ni muda mfupi tu unakaa kituoni gari linakuja unaondoka, kwetu hii ni neema."

Pia Joseph Mkopa, mtumiaji wa usafiri huo alisema: "Hakuna purukushani kwa siku ya leo ikilinganishwa na siku zingine ambazo foleni ilikuwa kubwa, abiria tunaingia kwenye usafiri kwa utaratibu jambo ambalo walikuwa wanakosea ni kutuacha tuwe wengi eneo moja."

Hata Christina Mrosso, mkazi wa Ubungo, hakuwa mbali na wenzake, yeye alisema kwa hali aliyoiona ya usafiri, anafikiria kuanza kuacha kutumia gari binafsi.

"Naishi Ubungo, shughuli zangu nafanya Kariakoo, ahueni ya usafiri ikiendelea nitaacha gari nyumbani kwani haitakuwa na haja, pia nitapunguza gharama," amesema.

Anuari Kasmini, alisema kuna haja ya wafanyabiashara kuangalia namna ya kuanzisha maegesho ya magari mwishoni mwa vituo vya mabasi.

Japhet John, mkazi wa Mbezi amezishauri mamlaka zitumie fursa hii kusimamia moja kwa moja utaratibu wa kuingia kwenye magari kwa foleni na kuondokana na utamaduni wa ovyo uliozoeleka wa kugombea mabasi.

"Mbona pale Mbezi tumeshazoea kupanga foleni, hata kule Muhimbili watu wanapamba foleni, kwa nini isiwe Kimara, Kariakoo, Ubungo au Feri?" amehoji.

***Imeandikwa na Peter Elias, Nasra Abdallah na Baraka Loshilaa***

# Sintofahamu yatanda wafanyakazi kiwanda cha chai Rungwe

Sadam Sadick, Mwananchi
ssadick@mwananchi.co.tz

**Mbeya.** Taharuki imetanda kiwanda cha Wakulima wa Chai kilichopo Katumba wilayani Rungwe mkoani Mbeya kufuatia wafanyakazi 216 kuandamana kwa mabango kupinga kufukuzwa kazi wakidai stahiki zao, huku wakiiomba Serikali kuingilia kati.

Imeelezwa kuwa tangu kufungwa kwa kiwanda hicho Mei 9 mwaka huu, zaidi ya wakulima 15,000 wameathirika na baadhi wameanza kutelekeza mashamba yao na wengine kuhamia kilimo cha mazao mengine na kuathiri uchumi wa Wilaya hiyo.

Wakizungumza jana wakati wa maandamano hayo, wafanyakazi hao walisema msimamo wao ni kuendelea na kazi hadi waajiri wao Tatepa na Maris Afrika (wawekezaji kiwandani hapo) watakapowalipa stahiki zao zaidi ya Sh2.17 bilioni.

Mwenyekiti wa kamati ya madai ya wafanyakazi kiwandani hapo, Robert Shayo alisema barua waliyopokea kutoka kwa waajiri kufukuzwa kazi imeibua mshtuko na sintofahamu.

Alisema jumla ya wafanyakazi 216 ndio walipokea barua ya kufukuzwa kazi, wakidaiwa hadi Septemba 30 wawe wameondoka ofisini, kinyume na makubaliano ya mkataba.

"Msimamo ni kubaki hapa kazini, tunadai mafao NSSF, madai ya likizo na malipo mengine ya kisheria kwa mujibu wa mkataba kazini, wametushtukiza sana," alisema Shayo.

Kuhusu kuendelea kubaki kazini ilhali barua inawataka kuondoka, Shayo alisema gharama zitaongezeka kisheria kwa kuwa kumekuwapo kukiuka utaratibu wa kuwaondoa kazini.

Meneja wa kiwanda hicho, Stanslaus Benela alisema hawapo tayari kuondoka kazini, akieleza kuwa tangu kufungwa kiwanda hicho imeathiri uchumi wa wananchi wa Rungwe na wakulima wenyewe na kushusha pato la Taifa.

**15,000**

**Idadi ya wakulima walioathirika na kufungwa kwa kiwanda cha chai Rungwe.**

Alisema hadi sasa wapo wakulima walioanza kutelekeza mashamba yao, wengine wakihamia kilimo cha mazao mengine kwa kung'oa chai akiomba Serikali kuingilia kati suala hilo ili kupata mwekezaji mpya.

"Wakulima zaidi ya 15,000 wameathirika, lakini uchumi wa wananchi na Wilaya hii kwa ujumla umeshuka na kuligusa Taifa kwa kuwa huduma ya maji na umeme bili hazilipwi, jamii iliyozunguka kiwanda nao wameguswa," alisema.

"Taasisi za kifedha ambazo zilikuwa hapa Rungwe zikipokea mishahara ya wafanyakazi na wakulima kupitishia malipo yao hakuna tena, mifuko ya hifadhi ya jamii nayo haipokei kitu," alisema meneja huyo.

Naye Katibu wa Umoja wa Wafanyakazi wa Kilimo mashambani Mkoa wa Mbeya (TPAWU), Jacline Novat alisema wamependekeza mwajiri kutoa mshahara wa msingi kwa mfanyakazi, malipo ya likizo, cheti cha utumishi, tuzo ya muda mrefu.

Alisema mwajiri pia aliombwa kulipa Sh500,000 kwa kila mfanyakazi kwa kutambua mchango wake, kodi ya nyumba ya miezi mitatu, na waajiriwa nje ya Tukuyu walipwe nauli zao.

"Kwa maana hiyo tunasubiri mrejesho kutoka kwa muajiri Jumatatu ya wiki ijayo ili tujue hatima yetu, kimsingi tuwe na uvumilivu kwa kuwa yupo mwakilishi wake ambaye atatupa taarifa," alisema Jacline.

CamScanner